# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Barabara ya Kilimatinde Cheyo,
S.L.P. 1020,
45112 TABORA,
Barua Pepe: rbctabora@pccb.go.tz.
**TANZANIA.**
www.pccb.go.tz

## TAARIFA YA UTENDAJI KAZI JANUARI 2020 HADI MACHI 2020

**TABORA – APRILI 15, 2020**

TAKUKURU Mkoa wa Tabora kwa kipindi cha Januari 2020 hadi Machi 2020 imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake tuliyokabidhiwa kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007.

Kazi mbali mbali zimefanyika katika madawati ya Uchunguzi, Elimu kwa Umma pamoja na Uzuiaji Rushwa.

**ELIMU KWA UMMA**

Katika upande wa kuelimisha jamii ili ishiriki kivitendo katika mapambano dhidi ya rushwa - Elimu ilitolewa kwa makundi mbalimbali ikiwemo vilabu vya wapinga rushwa katika shule za msingi, sekondari, vyuo, watumishi wa serikali na mashirika mbali mbali ya umma. Kazi ambazo zimefanyika ni pamoja na:-

- Semina **22,**
- Uandaaji wa makala **08**,
- Mikutano ya hadhara na mijadala ya wazi **26,**
- Utoaji wa habari na vipindi redioni **03.**
- Kuimarisha na kufungua vilabu vya wapinga rushwa **68,**
- Kushirki katika maonesho **02**

**UZUIAJI RUSHWA**

Dawati la uzuiaji rushwa lina majukumu makuu mawili ambayo ni ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo na uchambuzi wa mifumo. Majukumu yote haya mawili yana lengo la kuweza kubaini uwepo wa

viashiria au vitendo vya rushwa ili kuweza kuchunguza na au kushauri mamlaka husika namna bora ya kuziba mianya ya rushwa.

**Ufuatiliaji wa Miradi ya maendeleo**

Kwa Kipindi cha Januari 2020 hadi Machi 2020, tumefuatilia miradi ya maendeleo kumi na nane (18) yenye thamani ya Shilingi 522,072,250.17 katika sekta za Elimu (ujenzi wa madarasa katika shule za sekondari na msingi), Afya na Barabara. Kupitia ufuatiliaji huu, tumebaini viashiria vya ukiukwaji wa taratibu kwenye utekelezaji wa mradi mmoja kwenye sekta ya elimu ambao uchunguzi wake unaendelea na ikiwa kutakua na ubadhirifu wowote wahusika watafikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili.

**Uchambuzi wa Mifumo**

TAKUKURU inafanya uchambuzi wa mifumo ili kuweza kubaini mianya ya rushwa na kushauri mamlaka husika namna bora ya kuiziba mianya hiyo. Katika kipindi husika, tulifanya uchambuzi katika zoezi la ulipwaji wa fedha za wakulima wa pamba, uendeshaji wa vyama vya ushirika na uchambuzi katika usimamizi wa mapori tengefu.

Aidha tumefanya warsha na wadau kwa lengo la kujadili na kukubaliana mikakati ya udhibiti wa mianya ya rushwa katika manunuzi ya umma na warsha katika mfumo wa matumizi ya fedha za capitation grants mashuleni.

## UCHUNGUZI NA MASHTAKA

Katika kipindi husika, TAKUKURU Mkoa wa Tabora imepokea na kufanyia uchunguzi tuhuma mbalimbali za rushwa kwa mchanganuo ufuatao.

- Tumepokea taarifa 105 za malalamiko. Kati ya taarifa hizo taarifa 53 zilihusu makosa ya rushwa na taarifa 52 Zilihusu makosa mengine yasiyohusiana na rushwa.
- Tumekamilisha uchunguzi wa majalada kumi na tatu (13)
- Tumefungua kesi mpya tano (5) Mahakamani
- Kesi (3) zimetolewa maamuzi na kushinda. Kesi tulizoshinda ni pamoja na kesi inayomhusu mhudumu wa afya Hospitali ya Kitete Bw Nestory Michael aliyeomba rushwa kwa ndugu wa mgonjwa ili aweze kupatiwa damu, kesi nyingine ilihusu Maafisa wa wa kampuni ya udalali Mikidadi Abdallah Hepautwa walioomba rushwa ili wasiuze nyumba ya mteja aliyekuwa anadaiwa na Benki na kesi ya tatu ilihusu mwenyekiti wa Kijiji Bw Charles Luwambo aliyeomba rushwa kwa aliyekuwa akidaiwa kummua mkewe ili asifikishwe polisi.
- Jumla ya mashauri ishirini na mbili (22) bado yanaendelea mahakamani

Kuanzia Januari 2020 hadi Machi 2020 TAKUKURU Mkoa wa Tabora kupitia operesheni zake, imefanikiwa kuokoa fedha jumla ya shilingi 118,609,927/- (**milioni mia moja kumi na nane laki sita**

**na tisa mia tisa ishirini na saba tu**) katika maeneo mbalimbali ikiwemo kwenye miradi ya maendeleo, vyama vya ushirika na watu binafsi.

- Kati ya fedha zilizookolewa TAKUKURU imefanikiwa kuwarejeshea walimu wastaafu wawili fedha taslimu na nyumba baada ya kubani kuwepo dhuluma inayofanywa kwenye **MIKOPO UMIZA** na wakopeshaji. Jumla ya Sh. 41,200,000 zimerejeshwa kwa mwalimu mstaafu Wilaya ya Kaliua na nyumba moja yenye thamani ya sh 15,000,000 imerejeshwa kwa mwalimu mstaafu wilaya ya Sikonge.

- Aidha TAKUKURU Tabora imechunguza na kurejesha fedha zilizokusanywa kwa POS na kufanyiwa ubadhirifu wilaya ya Igunga kiasi cha Shs 32,041,800 fedha hizo zimerejeshwa kwenye akaunti ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga.

- Vilevile TAKUKURU imerejesha kiasi cha Shs 1,000,000/= (Milioni moja tu) fedha alizolipwa mganga mfawidhi wa Zahanati ya TUTUO Wilaya ya Sikonge, ambazo zilikuwa ni fedha za ukarabati wa kisima alizolipwa kinyume na taratibu.

- Tunaendelea kusimamia urejeshwaji wa fedha ya vyama vya ushirika (AMCOS) na SACCOS ambapo hadi sasa baadhi ya wakulima tayari wameshalipwa fedha zao na fedha zingine zimehifadhiwa kwenye akaunti ya serikali kwa ajili ya kuandaa utaratibu wa kuwalipa wakulima na kurejeshwa kwenye vyama husika.

**MIKAKATI TULIYOJIWEKEA KWA KIPINDI CHA APRILI HADI JUNI 2020**

TAKUKURU mkoa wa Tabora itaendelea na utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007.

Mkazo utawekwa katika kuelimisha na kuzuia vitendo vya rushwa katika jamii hasa Rushwa kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Madiwani, Wabunge na Rais utakaofanyika Oktoba 2020. Hii itafanyika kwa lengo la kuhakikisha wananchi na wagombea hawajihusishi na vitendo vya Rushwa na wanapatikana viongozi wenye maadili na uzalendo kwa Taifa lao.

Aidha TAKUKURU mkoa wa Tabora tunatambua kuwa kuna baadhi ya wanasisa wameanza kujipitisha na kuomba uungwaji mkono kwenye uchaguzi ujao. Tunawataka wananchi wote na wanasiasa katika mkoa wetu wa Tabora kufuata taratibu na sheria za nchi. Yeyote atakaebainika kujihusha na uvunjifu wa sheria kama vile kuanza kampeni kabla ya wakati atachukuliwa hatua kali.

Napenda kuwashukuru waandishi wa habari kwa namna mnavyohabarisha jamii kuhusu madhara ya rushwa asanteni sana.

Aidha nawashukuru wananchi wote wa mkoa wa Tabora kwa ushirikiano mnaotoa kwa TAKUKURU, niwakumbushe wananchi kwamba wanalo jukumu la kushirikiana na TAKUKURU katika kutoa taarifa juu ya vitedo vya rushwa vinanvyojitokeza katika maeneo yao na kwa sasa tumeboresha zaidi ukusanyaji wa Taarifa kupitia matumizi ya TAKUKURU APP, itakayowawezesha wananchi kutoa taarifa za vitendo vya Rushwa kwa kurekodi sauti, kupiga picha au kuchukua video ya tukio husika na kuiwasilisha TAKUKURU ili hatua stahiki zichukuliwe.

Vilevile, natumia fursa hii kuwatahadharisha wananchi wa mkoa wa Tabora kuwa hivi karibuni kumejitokeza matapeli wanaowarubuni wananchi kwa kuwapigia simu na kuwataka waripoti ofisi ya TAKUKURU mkoa wa Tabora, au Makao Makuu Dodoma na baadae huwaomba rushwa. Tunawatahadharisha wananchi msikubali kutoa rushwa. TAKUKURU ina ofisi katika kila mkoa na kila Wilaya hivyo ukipigiwa simu kabla ya kusafiri kwenda kituo husika jiridhishe kuhusu wito huo kutoka kwenye ofisi ya TAKUKURU iliyo karibu au kwa kupiga nambari ya dharura 113 BURE.

***Asanteni sana***

Imetolewa na:
Musa Chaulo
**MKUU WA TAKUKURU (M) TABORA**